

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
KITENGO CHA KUDHIBITI FEDHA HARAMU**

Simu Nambari: +255 22 2129457

Nukushi: +255 22 2129471

Tovuti: <http://www.fiu.go.tz>

Barua pepe: info@fiu.go.tz

(Mawasiliano yote ya kiofisi  
yaandikwe kwa Kamishna na  
siyo kwa mtu binafsi).

Nukushi: +255 22 2129471



1 Mtaa wa Madaraka  
S.L. P. 5145,  
**11468 DAR ES SALAAM  
TANZANIA**

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

Wananchi wote mnatangaziwa kuwa kutakuwa na mnada wa hadhara wa vifaa mbalimbali chakavu siku ya **jumanne tarehe 16.07.2024** katika eneo la Wizara ya Fedha, Mtaa wa Madaraka -Dar es Salaam.

**Masharti ya mnada:-**

1. Chombo kitauzwa kama kilivyo mahali kilipo.
2. Mnunuzi atalazimika kulipa papo hapo gharama isiyopungua asilimia mia moja (100%) ya thamani ya chombo / kifaa alichonunua siku ya mnada. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti hili atakosa haki zote za ununuzi wa chombo/kifaa husika na hatua kali zitachukuliwa dhidi yake kwa mujibu wa sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwani ataonekana kama mwenye kutaka kuharibu mnada.
3. Mnunuzi atatakiwa kuondoa au kuchukua chombo alichonunua siku ya mnada baada ya kukamilisha malipo.
4. Ruhusa ya kuangalia vyombo itakuwa siku mbili kabla ya tarehe ya mnada

Wote mnakaribishwa



KAMISHNA